

CHIMBUKO LA METHALI KATIKA KINAANDI

Naomi C. Jescah
Chuo Kikuu cha Moi
jessnamc@gmail.com

na
Biwott K. Anthony
Chuo Kikuu cha Moi
biwott1@gmail.com

Ikisiri

Makala hii itaangazia chimbuko la “kalewenoik” yaani methali za Kinaandi huku ikijaribu kubainisha hadhira iliyotungiwa methali hizo na utendakazi wake. Aidh, baadhi ya methali zitafsiriwa na kufafanuliwa maana na matumizi katika jamii, uhusiano wake na methali za Kiswahili utachunguzwa. Mwishowe tutaendesha mjadala utakaojaribu kubainisha iwapo methali hizi zingali na umuhimu katika jamii ya Kinaandi katika karne ya 21 ambapo pamekuwa na mabadiliko mengi katika jamii yaliyosababishwa na dini, ukoloni mamboleo na hata utandawazi.